**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**TUKUYU TEACHERS COLLEGE**

**P.O BOX 554 Tukuyu. Phone: 025 2552357, 0782666172/0718278525**

**Email address: tukuyutc@gmail.com / tukuyutc@moe.go.tz.**

---

***KUMB.NA /TKY/JOI/*** **VOL.II/24**

**Ndugu …………………………………………….**

**………………………………………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UALIMU YA STASHAHADA MAALUM ELIMU YA MSINGI MWAKA WA MASOMO 2024/2025**

1. **Utangulizi**

Ninayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa na Wizara ya Elimu,Sayansi na Teknolojia kujiunga na mafunzo ya Ualimu ya **Stashahada maalum ya Ualimu Elimu ya Msingi** katika Chuo cha Ualimu Tukuyu kwa mwaka wa masomo **2024/2025.** ***Hongera sana!*** Moto wa Chuo chetu ni **ELIMU NI KAZI.**

2. **Mahali Chuo Kilipo**

Chuo kipo mkoani Mbeya, wilaya ya Rungwe, umbali wa ***kilometa 73*** kutoka Mbeya mjini. Chuo kipo Tukuyu mjini, mtaa wa Msasani umbali wa ***km 2*** kutoka stendi kuu ya mabasi.

3. **Kuripoti Chuoni**

Unatakiwa kuripoti chuoni tarehe **09.09.2024. Utahitajika** kuhudhuria mafunzo kabilishi ***(Orientation Course)*** yatakayoanza mara moja. **Ukichelewa kwa muda wa majuma mawili hautapokelewa.**

4. **Mafunzo Yatolewayo Chuoni**

Chuo kinatoa mafunzo ya Stashahada Maalumu ya Ualimu katika masomo ya Sayansi, Hisabati na Tehama (Special Diploma in Science, Mathematics and ICT) ambayo yanajumuisha masomo ya Fizikia, Kemia, Bailojia, Hisabati na Tehama.

Kila mwanachuo atasoma tahasusi kama alivyopangiwa na Wizara pamoja na masomo ya ualimu. Maelekezo zaidi yatatolewa wakati wa mafunzo kabilishi. Katika kipindi chote cha mafunzo, kila mwanachuo atatakiwa kufaulu mazoezi ya darasani na mitihani mbalimbali itakayotolewa.

5. **MAHITAJI KWA AJILI YA USAJILI**

Wakati wa usajili utatakiwa kuwasilisha nyaraka/viambata vifuatavyo:

## 5.1 VYETI NA VITAMBULISHO

- Barua ya kukuita chuoni
- Cheti cha kuzaliwa
- Vyeti **halisi** vya kidato cha **IV (Academic & Leaving Certificates)** na vyeti vingine ulivyosomea na vivuli vyake, nakala tatu kila kimoja.
- Kitambulisho chenye picha na jina lako (mf. cha Mpiga kura, hati ya kusafiria, kitambulisho cha uraia au leseni ya udereva)

## 5.2 ADA

Ada ya Mafunzo ni **Tshs. 450,000/=** kwa mwaka. Fedha hizi zinaweza kulipwa mara moja kwa mwaka (Tshs. 450,000/=) au kwa awamu mbili Tshs. 225,000/= kwa kila nusu mwaka. Fedha ya ada italipwa kwenye mfuko Mkuu wa Serikali baada ya kutengenezewa control number na Mhasibu wa chuo. Malipo yanaweza kufanyika ukiwa nyumbani baada ya kuomba na kutengenezewa *control number* kutoka kwa mhasibu. Namba ya mawasiliano tumia 0766484535 kwa ajili ya kutengenezewa control *number*

**Jinsi ya kufanya malipo ya ada:**

a) Kupitia Benki au wakala wa benki yoyote

b) Kupitia mitandao ya simu

## 5.3 MICHANGO

a) Huduma ya kwanza (matibabu) Tshs. **10,000/=** kwa mwaka.

b) Usajili na kitambulisho **Tshs. 20,000/=** inalipwa mara moja mwaka wa kwanza.

c) Serikali ya WanachuoTshs. **5,000/=** kwa mwaka.

d) Kukodi godoroTshs. **10,000/=** kwa mwaka.

e) Ukarabati Tshs. **25,000/=** (kwa mwaka).

f) Elimu ya Michezo Tshs. **30,000/=** kwa mwaka.

g) Ulinzi **30,000/=** kwa mwaka.

h) Usafi, mazingira na elimu ya kujitegemea **20,000/=** kwa mwaka.

i) Bima ya afya **50,400/=** kwa mwaka na italipwa mhula wa kwanza (***kwa wale walio na Bima ya Afya ya Taifa (NHIF) hawatalazimika kulipa tena,na ni lazima aje nayo***).

j) T – Shirt yenye Nembo ya Chuo Tshs. **15,000/=** inapatikana chuoni

**Jumla ya michango inayotakiwa kulipwa ni Tshs. 215,400.00**

**Muhimu:**

(i) ***Fedha za michango*** zilipwe benki ya ***NMB (***Tukuyu TC Gen**. A/C No. 61401000011*)***

(ii) Uje na hati halisi ya malipo ya benki (original pay slip) **ikionesha** kiasi kilicholipwa na yenye **jina kamili la mwanachuo**.

(iii) **Usichanganye malipo ya ada na michango kwenye akaunti moja** wala fedha yako ya matumizi isiwekwe katika akaunti ya chuo

iv) Uje na Ream moja A4 ya karatasi 500 nyeupe kwa muhula

**6. SARE**

**Wanaume**

- **Suti** (Suruali mbili na koti), rangi ya bluu nyeusi **(darkblue).**
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba, vya kufunika na vyenye visigino vifupi na soksi nyeusi
- Tai ndefu inayofanana na rangi ya suruali.
- Koti jeupe la maabara.

**Wanawake**

- Suti ya rangi ya bluu nyeusi **(darkblue)** (sketi mbili na koti).
- Mshono wa sketi uwe ni wa **solo isiyobana ndefu hadi kwenye vifundo viwili vya miguu.**
- Mashati mawili meupe ya mikono mirefu.
- Viatu vyeusi vya kufunika, vya kamba na vyenye visigino vifupi na soksi nyeupe.
- *Neck tie scarf* inayofana na rangi ya sketi.

Angalia mchoro





- Koti jeupe la maabara
- **Kwa watakaovaa Hijab**: ushungi mweupe mrefu unaoficha viwiko vya mikono na usioangaza (trasnsparent) na koti la rangi ya ***(darkblue).***

(kwa mashono ya sare angalia ilivyo katika michoro na 1 & 2)

**PICHA 1**

**PICHA 2**

**7. MAVAZI MENGINE MUHIMU**

i. Mavazi kwa ajili ya Michezo

- **Track Suit** bluu nyeusi( **darkblue**)
- Raba nyeupe na soksi
- T-shirt rangi nyekundu au njano (isiwe na maandishi)

ii.**Mavazi mengine yasiyo rasmi**

Kwa wakati mwingine wowote utatakiwa kuvaa mavazi ya heshima na yenye maadili ya kiualimu. **Mavazi ya kubana**, **jeans, kaptura (pensi) vimini, vitop na mavazi ya kufanana na hayo hayaruhusiwi.**

**8. MAHITAJI MUHIMU KWA AJILI YA MALAZI**

- Kwakuwa hali ya hewa ni ya baridi na mvua za mara kwa mara karibu mwaka mzima unashauriwa kuja na blanketi moja na shuka mbili (pink kwa wasichna na bluu kwa wavulana), mto na foronya .
- Vyombo vya kulia chakula na ndoo.
- Dumu la kuhifadhia maji ya kunywa (ujazo wa lita 5).

**9. MAHITAJI YA LAZIMA KWA AJILI YA TAALUMA**

- Madaftari makubwa ya kutosha (masomo kumi)
- Majalada matupu (flat files) kwa ajili ya mkoba wa kazi (Portifolio) kwa kila somo.
- Mihutasari miwili ya shule ya Msingi kwa masomo yako ya mchepuo.
- Vitabu viwili vya kiada (text books) kwa masomo yako ya mchepuo.
- Mathematical set na koti jeupe la maabara.
- Non programmable scientific calculator (fx 991)

**10. MAAGIZO MUHIMU KWA AJILI YA AFYA YA MWANACHUO**

Unatakiwa kuzingatia yafuatayo kwa ajili ya ustawi wa afya yako kwa kipindi chote cha mafunzo :

Uje na fomu ya afya (iliyoambatanishwa) ikiwa imejazwa kikamilifu na mganga wa hospitali /kituo cha afya kinachotambuliwa na Seri kali, ili kuthibitisha hali ya afya yako.

- Kwa wenye matatizo /mahitaji maalumu uje na uthibitisho wa daktari. **NB : Chuo hakitoi chakula maalumu (*Special diet).***

**11. MWISHO:**

**Ualimu bora huanzia chuoni,** hivyo, baada ya kusajiliwa utapitishwa katika Sheria, taratibu na ***Kanuni za Mwenendo Bora wa Mwanachuo*** ambapo utatakiwa kujaza fomu maalum kuthibitisha kuwa utazifuata wakati wote wa mafunzo.

Kwa mawasiliano zaidi tumia namba za simu zilizooneshwa kwenye anwani.

Karibu sana!

**Shamila I. Makau**

**MKUU WA CHUO**

MKUU WA CHUO
CHUO CHA UALIMU TUKUYU
S.L.P. 534 TUKUYU

1. Katibu Mkuu,
   Wizara ya Elimu,Sayansi naTeknolojia ,
   Mji wa Serikali,Eneo la Mtumba ,
   Mtaa wa afya,
   S.L.P 10
   **40479 DODOMA**.
2. Mdhibiti Mkuu wa Shule Kanda ya Nyanda za Juu Kusini
   S.L.P 92,
   **MBEYA**
3. Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Chuo
   S.L.P 993
   Mbeya

**GOVERNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

TO: The Medical Officer
Tukuyu Teachers' College.

From: Principal
P.O. BOX 554, TUKUYU

**……………………………………….**
**……………………………………….**

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time teacher's course.

A: 1. (a) Eye – sight
(b) Hearing
(c) Speech
(d) Venereal Diseases
(e) Leprosy
(f) Limbs
(g) Epilepsy
2.Neuroses
3.Other serious diseases.

B: Blood Group

Date: ……………………..  Signature…………………………

Official Stamp

*************************************************************************

**PART B: MEDICAL CERTIFICATE.**

(To be completed by Government Medical Officer)

I have examined the above-named student that he/she is physically fit/unfit and mentally *fit/unfit for a full-time teacher Education course.

- (a) Eye – sight……………………………………………………………………
  (b) Hearing…………………………………………………………………...
  (c) Limbs……………………………………………………………………...
  (d) Speech……………………………………………………………………….
  (e) Leprosy…………………………………………………………………....

II. Neuroses……………………………………………………………………………….
III. Other serious diseases……………………………………………………………….….
IV. pregnancy………………………………………………………………………………

**Date……………………………………...Signature…………………………………….**

**Official Stamp**